TANGAZO LA SERIKALI NA. 959 la tarehe 29/11/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA KYOSA KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA WA KYOSA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Kyosa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kyosa ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kyosa.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza eneo la Msitu wa Kyosa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa ni-
(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, nyasi, miti ya miombo, vyanzo vya maji na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na
(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote

inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kyosa.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kuanzisha Msitu wa Hifadhi wa Taifa Kyosa, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

---

JEDWALI

---


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA ILEJE NA RUNGWE

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA KYOSA

Makadirio ya eneo: Hekta 1060.070 au Kilometa za Mraba 10.60 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Kyosa unaopatikana Wilaya ya Ileje na Rungwe, Mkoa wa Songwe kama lilivyochorwa katika Ramani Jb 2933 (Skeli 1:10,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*